

JINA.....NAMBA YAKO..... TAREHE.....

SHULE..... SAHIHI YA MTAHINIWA.....

102/3

KISWAHILI

Karatasi ya Tatu

Fasihi

Saa:2 ½

**TATHMINI YA PAMOJA KCSE
WILAYA ZA KISUMU KASKAZINI NA MASHARIKI
JULAI / AGOSTI 2010**

MAAGIZO

- ❖ *Jibu maswali **manne** pekee.*
- ❖ *Swali la kwanza ni la **lazima**.*
- ❖ *Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki yaani :Ushairi, Tamthilia, Fasihi simulizi na Riwaya.*
- ❖ ***Usijibu** maswali mawili kutoka sehemu moja.*

HADITHI FUPI K.W.Wamitila.

1. Lazima

Sikiza Muus, kama ni hivyo vihela vyako, ninaweza kukurudishia. Wewe huoni kwamba ni lazima tumshtue kidogo? Sharti atuheshimu.

- a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4).
- b) Neno “tumshtue kidogo,” ni kinaya. Jadili. (alama 6)
- c) “Majuto ni mjukuu”.ni methali inayoafiki dondoo hili. Jadili. (alama 10).

TAMTHILIA *Kithaka wa Mberia:Kifo kisimani.*

Jibu swali la 2 au la 3.

2. Eleza tofauti iliyokuwepo kati ya uongozi wa Mtemi Bokono na Mtemi Mlima.

(alama 20)

3.Alaa! unataka pia kuwa mshairi! Ukitaka kuwa mshairi stadi, jifunze mbinu zaidi za kishairi, tashbihi pekee haitoshi!

- a) Fafanua muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
- b) Wahusika wana msimamo tofauti kuhusu wanachokizungumzia.Thibitisha msimamo wa kila mmoja wao. (alama 4)
- c) Ni tashbihi ipi aliyokuwa ametumia mzungumzaji? (alama 2)
- d) Ni kwa nini mzungumzaji anastahili lawama. (alama 10)

USHAIRI Soma shairi hili kisha ujibu maswali yanayofuata.

4. Matapeli : Kuvuna S.

Salamu naanza mimi, niwajuyeye walimwengu

Muyatege masikiyo, uneni pate lipuka

Pia mutiye manani, asilani musipuze

Kina matapeli ndugu, hutokea kama njozi.

Wanooitwa matapeli, hao watu walaghai

Wonapo pato unalo, kukupoka hutamani

Wataja kufanya zuzu, japo wewe mashuhuri

Kina matapeli ndugu, hutokea kama njozi.

Taja jaye mfadhili, kukuauni kutaka
La ajabu keshajua, ya kwako yanokutasa
Takonea imaniye, budi kumwamini huna
Kina matapeli ndugu, hutokea kama njozi.

Ndugu na wakakupanga, kumbe ni ndugu bandia
Ya ulimi takulisha, rohoyo kuiridhisha
Nawe tapata msiri, ya moyoni funulia
Kina matapeli ndugu, hutokea kama njozi

Kama kinyonga wataja, mpate afikiana
Ulimi tawa laini, mithiliye malaika
Nawe taona ni mwema, wake mfano hapana
Kina matapeli ndugu, hutokea kama njozi

Ama taja kama chui, walovaa ya kondoo
Machoyo tafumba ndi, hatimaye takunyoa
Nawe punde kilevuka, hayupo keshayoyoma
Kina matapeli ndugu, hutokea kama njozi

Hawa matapeli jama, ni bora kuwaambaa
Ngawaje vigumu huwa, kwayo hila wanavyoja
Kweli ndugu jihadhari, sije wakakuhadaa
Kina matapeli ndugu, hutokea kama njozi

Maswali

- a) Eleza dhamira ya shairi hili. (alama 2)
- b) kwa kutoa mifano eleza aina tatu za idhini ya kishairi alizotumia mshairi. (alama 6)
- c) Andika ubeti wa nne kwa lugha nathari. (alama 4)
- d) Chambua muundo wa shairi katika ubeti wa tamati. (alama 4)
- e) Kwa kutoa mifano taja tamathali mbili za lugha zilizotumika katika shairi hili. (alama 4)

RIWAYA: S.A MOHAMMED: Utengano.Jibu swali la tano au la sita

5. Ni hatari tupu siku hizi, tunasakwa kila upande, basi hizi kelele zitatuchongea wenyewe.
- a)Kauli hii imetolewa katika muktadha gani ? (alama 4)
- b)Ni hatari gani anayoizungumzia ? (alama 4)
- c)Thibitisha kuwa wanawake “wamejichongea wenyewe” katika masuala yanayowakabili kwenye jumuiya ya utengano (alama 12)
6. Mwiba wa kujichoma hauna kilio.Onyesha jinsi methali hii inavyoana na yaliyomo katika riwaya ya utengano. (alama 20)

FASIHI SIMULIZI

7. a) Eleza maana ya misimu. (alama 2)
- b) Eleza sifa sita za misimu. (alama 6)
- c) Huku ukitoa mifano mwafaka fafania muundo wa nyimbo. (alama 8)
- d) Taja sifa zozote mbili za ulumbi. (alama 2)
- e) Ni nini umuhimi wa ulumbi. (alama 2)